FOMU YA IDHINI YA DATA NYETI ZA BAYOMETRIKI YA WORLDCOIN

**Muhtasari Mfupi.**

Muhtasari huu unakusudiwa kukusaidia kuelewa kwa haraka kile ambacho unaombwa kukubali unapojisajili kwenye kifaa cha Orb. Ikiwa unahitaji maelezo zaidi, unaweza kupitia maelezo kamili ya idhini, yaliyo hapa chini.

**Si lazima ukubaliane na Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti ili kushiriki katika Worldcoin.**

Haya ndiyo machaguo yako:

| **Machaguo** | **Athari** | **Maelezo** |
|---|---|---|
| **#1.**<br><br>**Sikubaliani na Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti** | Data Chache Zaidi Kukusanywa, lakini Utendaji Mchache Zaidi | Unaweza kutengeneza akaunti na kuwa na pochi la Worldcoin, lakini hautaweza kushiriki katika vipengele fulani vya Worldcoin, kama vile kupokea kiwango kidogo cha WLD bila malipo au kuwa na utambulisho wa kipekee na unaohamishika wa kidijitali. Kama tu kila mtumiaji wa Worldcoin, ni lazima ukubaliane na Kauli ya Faragha na Sheria na Masharti ya Mtumiaji ya Worldcoin. |
| **#2.**<br><br>**Kubaliana na Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti, lakini Usiwezeshe ("Kukubali") Umiliki Data** | Data Zinakusanywa, Utendaji Kamili lakini kuna Baadhi ya Usumbufu | Unaturuhusu **kuchukua picha za viini vya macho, macho, na uso wako** unapojisajili kwenye kifaa cha Orb. Data za picha zinafutwa baada ya kifaa cha Orb kutengeneza IrisCode kilingana na picha ya kiini cha jicho lako. Hatuhifadhi wala kuhamisha data za picha hadi kwenye hifadhidata yetu. Data za picha hazitaondoka kwenye kifaa cha Orb. Hata hivyo, unahitajika kuenda tena kwenye kifaa cha Orb ili IrisCode yako iweze kuthibitishwa tena tunaposasisha teknolojia yetu. |
| **#3.**<br><br>**Kubaliana na Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti na Uwezeshe ("Kukubali") Umiliki Data** | Data Zinakusanywa, Utendaji Kamili na kuna starehe zaidi | Unaturuhusu **kuchukua picha za viini vya macho, macho, na uso wako** unapojisajili kwenye kifaa cha Orb. Aidha, utaturuhusu kuhifadhi maelezo haya na **kutuma data hii kwa timu zetu** zilizo katika Umoja wa Ulaya (kwa sasa nchini Ujerumani na Polandi) na Marekani, kwa malengo ya kufunza teknolojia yetu, kama ilivyobainishwa hapa chini. Utakuwa na utendaji kamili na hautahitajika kuenda tena kwenye kifaa cha Orb kila wakati tunaposasisha teknolojia zetu, na pia utatusaidia kuenezesha Worldcoin ulimwenguni kwa haraka zaidi. |

**Unaweza kuondoa idhini yako ya Fomu ya Idhini ya Data Nyeti wakati wowote kwa kutumia lango letu la maombi linalopatikana kwenye anwani worldcoin.org/requestportal.**

**Hauwezi kupatiana maelezo yako ya bayometriki kwenye kifaa cha Orb bila kusoma hati kamili na kutia sahihi fomu ya idhini. Hauwezi kupatiana maelezo yako ya bayometriki kwenye kifaa cha Orb ikiwa wewe ni mkaazi wa jimbo la Illinois, Texas, au Washington au mji wa Portland, jimboni Oregon au mji wa Baltimore, jimboni Maryland.**

Tools for Humanity Corporation, pamoja na kampuni yake tanzu ya Ujerumani Tools for Humanity GmbH (kwa pamoja, "**TFH**" au "**sisi**"), inaongoza utenegenezaji wa mwanzo wa Worldcoin. Uchakataji wetu (ukusanyaji, utumiaji, uhifadhi, ufichuaji, na ufutaji) wa data zako za kibinafsi unatawaliwa na hati mbili: Kauli ya Faragha ya Worldcoin na Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti. Kauli ya Faragha inasimamia data zinazokusanywa kupitia tovuti, programu, na huduma nyingine za Worldcoin, nayo Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti za bayometriki inaelezea jinsi tunavyochakata data zako za bayometriki zilizokusanywa kupitia kifaa chetu cha Orb.Haki zako chini ya sheria husika ya faragha ya data zimebainishwa katika Kauli ya Faragha ya Worldcoin. Hati hizi zinaendanisha moja kwa moja, na zote mbili ni muhimu katika kuelewa jinsi faragha yako inayoathiriwa na kushiriki katika mradi wa Worldcoin. Kauli ya Faragha na Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti zimejumuishwa kwenye na kutawaliwa na Sheria na Masharti ya Mtumiaji ya Worldcoin.

Aidha, tunaambatana na misimamo iliyotajwa katika Kanuni Jumla ya Ulinzi wa Data (General Data Protection Regulation, "GDPR") za EU kwa masuala ya faragha. Kwa mfano, hata ikiwa nchi yako na sheria za faragha ya data ambazo ulinzi wake ni mchache kuliko GDPR, bado tunasindika data zako kulingana na GDPR. Pia tutatumia tu data zako kwa malengo yaliyotajwa hapa chini katika Sehemu ya 2.2 (na Sehemu ya 3.4 ukiwezesha Umiliki Data), hata ikiwa sheria za faragha ya data nchini mwako hazingezuia jinsi tunavyotumia data zako.

Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti za Bayometriki ina sehemu tatu:

1. Historia kuhusu mradi wa Worldcoin;
2. Idhini ya kusindika data nyeti; na
3. Kuwezesha Umiliki Data.

# 1. Historia.

### 1.1 Mradi wa Worldcoin

Mradi wa Worldcoin unalenga kuharakisha mpito wa kuelekea uchumi wa kiulimwengu unaohusha watu wote zaidi kwa kutengeneza teknolojia ya wavuti bila mamlaka kuu ("web3") ambayo ni kwanza kuwa ya kiulimwengu kabisa na inayotumika na watu wengi. "Worldcoin" ndilo jina linalotumika kwa sasa kwa teknolojia ya blockchain ambapo miamala inafanyika na pia jina la sarafu ya dijitali (limefupishwa kuwa "**WLD**"). Ili kufanya Worldcoin kufikiwa na ya haki, tutaruhusu kila mtu kuchukua mgao wake wa WLD bila malipo. Ili mradi huu upate mafanikio, ni lazima tuangazie tatizo la akaunti rudufu na ghushi mtandaoni (kama vile roboti), huku tukilinda faragha yako na usalama wa data zako. Kwa hilo, tumeamua kutumia picha za viini vya macho ili kutengeneza utambulisho wa kipekee wa wanadamu na, kwa upana zaidi, kutengeneza programu ambayo inaweza kuthibitisha uwepo wa mwanadamu kulingana na picha za viini vya macho. Unaweza kusoma mengi zaidi kuhusu mradi wa Worldcoin kwenye tovuti yetu (worldcoin.org).

### 1.2 Kifaa cha Orb

Ili kutekeleza uthibitishaji salama, tumetengeneza kifaa cha kipekee kinachoitwa **Orb**. Kinathibitisha kwamba wewe ni "mwanadamu wa kipekee" bila kukuhitaji upatiane hati zozote za utambulisho au maelezo mengine kuhusu wewe ni nani. Orb inapiga picha kadhaa za ubora wa juu zaidi za macho yako (haswa, viini vya macho yako) na uso wako (kichwa chako na mabega yako). Baadhi ya picha hizo zinatumika kuthibitisha wewe ni binadamu halisi, aliye hai. Zingine—kwa jina, za viini vya macho yako—zinageuzwa na kuwa **IrisCode,** msururu wa nambari ambao unatumiwa kubaini kana kwamba ulikuwa umejisajili tena hapo awali kwenye kifaa cha Orb.

# 2. Idhini ya Kuchakata Data Nyeti za Bayometriki.

**2.1 Data Tunazokusanya.**

Kwa idhini yako, tunakusanya data zifuatazo za bayometriki na za kibinafsi kwa kutumia kifaa cha Orb:

- **Picha za viini vya macho yako na macho yako.** Picha hizi zinapigwa kwa kutumia teknolojia ya "visible and near-infrared". Zinatumika kutengeneza IrisCode na kufunza teknolojia yetu ya kutambua na kutofautisha viini vya macho vya binadamu tofauti. Kama ilivyobainishwa katika Sehemu ya 2.3, hapa chini, teknolojia hii si timilifu na huenda ikafanya makosa, kama vile kubaini kimakosa kwamba tayari umejisajili kwenye kifaa cha Orb na umepata mgao wako wa WLD bila malipo.
- **Picha za uso wako.** Picha hizi zinapigwa kwa kutumia teknolojia ya "visible", "near-infrared", na "far-infrared". Pia tunapiga picha ya kina. Picha hizi zinatumika kuthibitisha kwamba wewe ni binadamu, na hivyo kusaidia kuzuia na kugundua ulaghai, na kufunza teknolojia.

**Muhimu!** Tunakusanya picha hizi ili kubaini kwamba wewe ni binadamu wa kipekee. Hata hivyo, hatutumii data hizi ili kujua wewe ni nani. Data za aina hii zinazingatiwa kuwa data za bayometriki zilizolindwa mali unakoishi na huenda zikawa chini ya ulinzi na vikwazo vya ziada.

**2.2 Tunachofanya na Data Hizi.**

Kwa idhini yako, tunatumia data zilizo hapa juu kwa malengo yafuatayo **pekee** (isipokuwa iwe umewezesha Umiliki Data, ulioelezewa hapa chini):

- Kutathmini IrisCodes;
- Kulinganisha IrisCode;
- Kuimarisha tathmini za IrisCode; na
- Kugundua kana kwamba mtumiaji ni binadamu na kana kwamba usajili ni halali (usalama na kuzuia ulaghai).

**2.3 Usahihi.**

Programu ya teknolojia inatumia uwezekano ili kubaini kana kwamba umejisajili kwenye kifaa cha Orb hapo awali. Si timilifu. Kwa hili, kinaweza kubainisha kimakosa kwamba tayari umejisajili kwenye kifaa cha Orb (na umepokea WLD bila malipo) hapo awali. Kwa wakati huu, hatuna njia ya watumiaji kuripoti hitilafu zinazotuhumiwa au kupinga uamuzi wa teknolojia. Ukikubaliana na Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti, unatupatia idhini yako ya uamuzi huu otomatiki.

**2.4 Si Lazima Uidhinishe Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti ili Kushiriki katika Worldcoin.**

Si lazima ukubaliane na Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti ili kushiriki katika Worldcoin. Bado unaweza kuunda akaunti na kuwa na pochi la Worldcoin bila kupatiana idhini hii, ingawa bado utahitajika kukubaliana na Sheria na Masharti ya Mtumiaji na Kauli ya Faragha ya Worldcoin. Aidha, ukichagua kutokubaliana na Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti za Bayometriki, basi hautaweza kushiriki katika vipengele fulani vya Worldcoin, kama vile kupokea kiwango kidogo cha WLD bila malipo au kuwa na utambulisho wa kipekee wa kidijitali.

**2.5 Kuondoa Idhini Yako**

Unaweza kuondoa idhini yako wakati wowote kwa kuwasiliana nasi kupitia:

**Lango la Maombi la Worldcoin kwenye tovuti ya worldcoin.org/requestportal**, au

**548 Market Street, PMB 49951, San Francisco, CA 94104 USA**

Pia unaweza kufuta data zako kutoka kwenye ndani ya programu ya Worldcoin chini ya menyu ya Mipangilio. Ukiondoa idhini yako, basi hatutatumia tena data zako kwa malengo yaliyotajwa hapa juu. Pia unaweza kuamua kufuta data zako kutoka kwenye ndani ya Worldcoin.

# 3. Kuwezesha Umiliki Data.

**3.1 Hadhi ya Sasa ya Mradi wa Worldcoin: Majaribio Nyanjani.**

Bado tunajitahidi kuboresha utendakazi wa Orb na kuimarisha mifumo ya maunzi ngumu na maunzi tepe ambayo inabaini kama mtu anastahiki kupokea mgao wa WLD bila malipo. Awamu hii ya utengenezaji tunaiita **Majaribio Nyanjani**.

Ili kuimarisha usahihi wa mfumo kubaini ustahiki, tunahitaji kuendela kufunza programu ya teknolojia yetu. "Kufunza" kunamaanisha kutumia picha kutoka kwa watu halisia kama wewe ili kusaidia programu "kujifunza" kutofautisha wanadamu na wasio wanadamu na kutofautisha mtu moja kati ya watu wengine wote. Huku programu ikifunzwa na kuwa bora zaidi, tutaisasisha mara kwa mara. Hili linapofanyika, huenda tukahitaji kuthibitisha tena utambulisho wako wa kipekee wa kidijitali, jambo ambalo litahitaji kutumia picha ya kiini cha jicho lako tena.

**3.2 Umiliki Data.**

Ukiidhinisha Fomu hii ya Idhini ya Data Nyeti za Bayometriki, katika programu ya Worldcoin utaombwa, "**Kuwezesha Umiliki Data**." Ukichagua kukubali Umiliki Data, utaturuhusu:

1. Kuhifadhi data nyeti zilizokusanywa na kifaa cha Orb wakati wa Majaribio Nyanjani;
2. Kutuma picha hizo kwa timu zetu zilizoko Umoja wa Ulaya na Marekani; na
3. Kutumia picha hizo kuendelea kutengeneza na kuimarisha programu, kama ilivyobainishwa hapa chini.

Kuna uwezekano kwamba hii itakusaidia kuepuka baadhi ya usumbufu kwa sababu, ikiwa tuna data za picha zako, basi hautahitaji kurudi kwenye kifaa cha Orb ili kuthibitisha tena utambulisho wako wa kidijitali tunaposasisha programu. Pia itatusaidia kwa sababu tunaweza kutumia data zako ili kufanya mfump kuwa bora zaidi na kueneza Worldcoin ulimwenguni kwa haraka zaidi. Kwa mara nyingine, si lazima Kuwezesha Umiliki Data, lakini kufanya hivyo kunaweza kukusaidia wewe pamoja nasi, na kwa hivyo tunashukuru sana.

**3.3 Data Tunayokusanya Unapowezesha Umiliki Data**.

Unapoidhinisha Fomu ya Idhini ya Data Nyeti, tunakusanya picha za viini vya macho yako na picha za uso wako, kama ilivyobainishwa katika Sehemu ya II.1 hapa juu. Data nyeti tunazokusanya hazibadiliki ikiwa utakubaliana na Umiliki Data.

**3.4 Tunachofanya na Data hizi Unapowezesha Umiliki Data.**

Unapokubaliana na Fomu ya Idhini ya Data Nyeti, tunatumia data zilizo hapa juu kwa malengo yaliyobainishwa katika Sehemu ya 2.2. Pia unapowezesha Umiliki Data, tunatumia data hizi kwa malengo ya ziada yafuatayo:

- Kusasisha IrisCode yako kwa njia otomatiki endapo tutasasiaha programu ya teknolojia yetu;
- Kutengeneza na kufunza teknolojia ya kutambua na kutofautisha viini vya macho vya binadamu tofauti;
- Kuondoa hitilafu kwenye teknolojia yetu ya kutambua viini vya macho;
- Kutengeneza na kufunza mfumo wa kugundua kama mtumiaji ni binadamu au kama usajili ni halali;
- Kutengeneza na kufunza miigo inayotumia picha za viini vya macho vya kutengenezwa kwa ajili ya mafunzo zaidi ya teknolojia; na
- Kufunza na kukutathmini wafanyakazi wanafanya kazi kwa kutumia mifumo hii.

**3.5 Utumaji Data, pamoja na Hatari Zinazoweza Kuwepo.**

Unapowezesha Umiliki Data, na hivyo kuturuhusu kutumia data zako kwa malengo yaliyoelezewa hapa juu katika Sehemu ya 3.4, kwa ujumla tunatuma data hizo kwa timu zetu za Utafiti na Utengenezaji (Research and Development, "**R&D**"), na hii inaweza kupelekea data zako kutumwa nje ya nchi ambako data hizo zilikusanywa. Timu hizi kwa sasa ziko katika Umoja wa Ulaya (kwa sasa nchini Ujerumani na Polandi) na Marekani. Kauli yetu ya Faragha inaelezea jinsi tunavyolinda na kuambatana na sheria za utumaji data nje ya mipaka. Sehemu ya 6 ya Kauli ya Faragha imebainisha hatari zinazohusiana na utumaji huo wa data nje ya mipaka.

Tunapopanga kuchapisha IrisCodes kwenye blockchain, hatutauza, kukodisha, kufanya biashara, au vinginevyo kufaidika kutokana na data zako za bayometriki. Hali nyingine chache ambapo tunaweza kushiriki data zako za bayometriki au data nyingine za kibinafsi zimefichuliwa kwenye Kauli yetu ya Faragha.

**3.6 Uhifadhi Data**.

Tutahifadhi picha zinazokusanywa na kifaa cha Orb, pamoja na data zako za bayometriki, mpaka tamatisho la utengenezaji na uboreshaji wa teknolojia au kama inavyohitajika na sheria au kanuni.

DCF20221010